JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU

UCHAGUZI WA WANAFUNZI WA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2022

Ndugu Wananchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekamilisha zoezi la uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka **2022.** Zoezi hilo limehusisha jumla ya wanafunzi **907,802** wakiwemo Wasichana **467,967** na Wavulana **439,835** ambao ni sawa na asilimia **81.97** ya wanafunzi waliofanya Mtihani wa Kuhitimu Elimu ya Msingi mwaka 2021. Kati ya waliofaulu na kupangiwa kujiunga na kidato cha kwanza wamo Wanafunzi wenye mahitaji maalum **2,673** sawa na asilimia **0.29** ambao kati yao wavulana ni **1,471** na wasichana **1,202**.

Kwa mwaka 2022 kumekuwa na **ongezeko la wanafunzi 73,932** sawa na asilimia **8.87** ya wanafunzi waliofaulu ukilinganisha na mwaka, 2020 ambapo jumla ya wanafunzi **833,872** walifaulu na kupata sifa ya kujiunga na masomo ya Kidato cha Kwanza.

Ndugu Wananchi, Mwaka huu kwa mara ya pili uchaguzi wa Wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Kwanza umefanyika kwa kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Uchaguzi wa Wanafunzi (*Students Selection-Management Information System*). Mfumo huu umesaidia mambo yafuatayo:

a) Kupunguza muda unaotumika kwenye uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na masomo ya Kidato cha Kwanza;

b) Kupunguza gharama zinazotumika wakati wa zoezi la uchaguzi na upangaji wa Wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Kwanza; na

c) Kuongeza ufanisi na uwazi katika uchaguzi wa wanafunzi kwa maana ya kuwa kila mwanafunzi anapangwa kwenye shule kulingana na Mwongozo wa Uchaguzi unavyoelekeza.

Ndugu Wananchi, Serikali ya Awamu ya 6 chini ya **Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilifanya maandalizi mapema kuhakikisha kuwa wanafunzi wote watakaofaulu Mtihani wa kumaliza darasa la saba mwaka 2021 wanajiunga na Elimu ya Sekondari ifikapo Januari, 2022. Kutokana na maandalizi hayo wanafunzi wote **907,802** waliofaulu Mtihani wa darasa la saba nchini mwaka 2021 wataanza masomo yao siku moja mara muhula wa masomo utakapoanza. **Na katika hatua hii natangaza kuwa muhula wa masomo kwa Shule za Msingi na Sekondari zinazomilikiwa na Serikali kwa mwaka 2022 utaanza tarehe 17 Januari 2022**.

Ndugu wananchi, Naomba nichukue fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kutilia mkazo suala la elimu ya sekondari, na kwa mara ya kwanza aliruhusu jumla ya **shilingi bilioni 240** kutumika kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya **madarasa 12,000** nchi nzima. Kabla ya uamuzi wa mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan wa kuongeza vyumba vya **madarasa 12,000**, shule za serikali za umma zilikuwa na **nafasi 430,604** kwa ajili ya kidato cha kwanza ambazo zinaachwa na wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne mwaka 2021. Ujenzi huu wa vyumba vipya vya **madarasa 12,000** utawezesha upatikanaji wa nafasi za nyongeza **600,000** na hivyo kuwa na **jumla ya nafasi 1,030,604** kwa ajili ya kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo 2022 na hii inaleta ziada ya nafasi 122,802 za kidato cha kwanza kulinganisha na wanafunzi waliofaulu ambao ni **907,802**.

Ndugu Wananchi, Vigezo vilivyotumika kuchagua wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Kwanza vimezingatiwa. Kigezo kikuu ni

Mwanafunzi kufikisha jumla ya alama za ufaulu kuanzia **121 hadi 300 kati ya alama 300**.

Shule zote za Sekondari za Bweni za Serikali ni za Kitaifa, hivyo wanafunzi wenye vigezo vya kuchaguliwa katika shule hizo hutoka Mikoa yote Tanzania Bara ili kuimarisha utaifa. Shule hizo zimegawanywa katika makundi matatu ambayo ni Shule za Sekondari za Bweni kwa wanafunzi wenye Ufaulu Mzuri zaidi, Shule za Sekondari za Bweni Ufundi na Shule za Sekondari za Bweni Kawaida. Utaratibu na vigezo vya kuwapangia wanafunzi katika shule hizo ni kama ifuatavyo.

a) **Shule za Sekondari za Bweni kwa Wanafunzi wenye ufaulu mzuri zaidi;** Nafasi katika shule za wanafunzi wenye ufaulu mzuri zaidi zimegawanywa kwa kila Mkoa kulingana na idadi ya watahiniwa wa Darasa la Saba waliosajiliwa katika Mkoa husika kwa kutumia Kanuni ya kugawa nafasi hizo kitaifa. Nafasi zilizotolewa kwa Mkoa zimegawanywa sawa kwa Halmashauri zote bila kujali idadi ya watahiniwa waliosajiliwa katika Halmashauri. Shule hizi zipo saba (7) ambazo ni **Msalato, Mzumbe, Kilakala, Kibaha, Ilboru, Tabora Wasichana na Tabora Wavulana**.

b) **Shule za Sekondari za Bweni Ufundi;** Nafasi katika shule za Sekondari za Ufundi zimegawanywa kwa kila Mkoa kulingana na idadi ya watahiniwa wa Darasa la Saba waliosajiliwa kwa Mkoa husika kwa kutumia Kanuni ya kugawa nafasi hizo kitaifa. Nafasi zilizotolewa kwa Mkoa zimegawanywa sawa kwa kila Halmashauri bila kujali idadi ya watahiniwa waliosajiliwa katika Halmashauri.

Aidha, Shule za Sekondari za Bweni za Ufundi zimeongezeka kutoka shule **7** zilizokuwepo awali ambazo ni **Tanga Tech, Moshi Tech, Musoma Tech, Bwiru Wavulana, Ifunda Tech, Iyunga Tech na Mtwara Tech** na kufikia shule **9** zilizopo sasa. Shule mbili za ufundi zinazotarajia kuanza mwaka 2022 ni **Shule ya Sekondari ya Ufundi Mwadui** iliyopo Mkoa wa Shinyanga na **Shule ya Sekondari ya Ufundi Chato**, Geita. Shule ya Sekondari ya Ufundi Mwadui ni shule ya Kwanza ya Ufundi kwa wasichana ambayo imepangiwa kuchukuwa wanafunzi wa bweni wasichana 80. Serikali imekamilisha maandalizi yote muhimu kwa shule hizo ikiwa ni pamoja na kuajiri walimu wa masomo ya ufundi, kuandaa mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji na kutenga bajeti ya fedha za ruzuku ya uendeshaji na ya chakula cha wanafunzi. Hivyo hatuna budi kuipongeza serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu kuanzisha shule hizo.

c) **Shule za Sekondari za Bweni Kawaida**; Nafasi katika Shule za Bweni za Kawaida za Kitaifa zimegawanywa kwa kila Halmashauri kwa kufuata idadi ya watahiniwa wa darasa la Saba waliotoka katika mazingira magumu tu kwa kutumia Kanuni ya kugawa nafasi hizo kitaifa. Katika kundi hilo, Wanafunzi kutoka Halmashauri za Majiji, Manispaa na Miji hawakuhusishwa isipokuwa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Ndugu Wananchi, Kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa hapo juu, wanafunzi **4,188** sawa na asilimia **0.46** wamechaguliwa kujiunga na shule za Bweni za Kitaifa, kwa mchanganuo ufuatao:

a) Wanafunzi **934** (Wavulana 514 na Wasichana 420) sawa na asilimia 0.1 wamechaguliwa kujiunga na Shule za Sekondari za wanafunzi wenye ufaulu mzuri zaidi:

b) Wanafunzi **1,265** (Wavulana 1,070 na Wasichana 195) sawa na asilimia 0.14 wamechaguliwa kwenda Shule za Sekondari za Ufundi:

c) Wanafunzi **1,989** (Wav 1,036 na Was 953) sawa na asilimia 0.22 wamechaguliwa kujiunga na Shule za Sekondari za Bweni Kawaida: na

d) Wanafunzi **903,614** (Wav 437,215 na Was 466,399) sawa na asilimia **99.54** wamechaguliwa kwenda shule za sekondari za kutwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Ndugu Wananchi, Serikali inatambua changamoto ya uhaba wa nafasi katika Shule za Bweni za Kitaifa hususan kwa wasichana. Napenda kuwahakikishia kuwa changamoto hiyo inafanyiwa kazi na tayari tumeanza kuchukua hatua za makusudi ili kuongeza nafasi katika shule za Bweni za Kitaifa kwa miaka ijayo. Hatua hizo ni pamoja na Kuanza upanuzi wa baadhi ya Shule Kongwe za Sekondari ambazo zinachukua wanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita pekee ili ziweze kuchukua pia wanafunzi wa Kidato cha Kwanza hadi cha Nne na kuharakisha ujenzi wa Shule mpya za Sekondari za Bweni kwa wasichana kupitia Mpango wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) ambapo kwa mwaka huu wa fedha tutajenga shule 10 kwa maana ya shule moja kila mkoa na tayari **shilingi bilioni 30 (bilioni 3 kila shule)** zimetengwa katika awamu ya kwanza ya ujenzi wa shule hizi.

Ndugu Wananchi, Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2022.

Aidha, nawashukuru Walimu, Wakuu wa Shule, Kamati za Shule, Maafisa Elimu Kata, Maafisa Elimu Wilaya na Mikoa pamoja na Viongozi wote wa Halmashauri na Mikoa na Wadau wa Elimu nchini kwa kutoa ushirikiano katika kusimamia uendeshaji na utoaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari nchini.

Aidha, napenda kuwaasa wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza katika shule za Sekondari za Serikali nchini kwa mwaka 2022, watumie vizuri fursa waliyoipata kusoma kwa bidii ili wafikie malengo waliojiwekea. Na ninawaagiza Walimu Wakuu wa Shule na Watendaji wa Elimu katika ngazi zote kuongeza bidii katika usimamizi na ufuatiliaji wa utoaji wa elimu ili kufikia malengo ya elimu yaliyowekwa na Serikali.

Ndugu Wananchi, kipeee narudia tena kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** kwa kutilia mkazo Elimu ya Sekondari, kwa mara ya kwanza aliruhusu kiasi cha shilingi **Bilioni 240** zitumike kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa **12,000** kwa mpigo ili kuwezesha wanafunzi wote waliofaulu kuanza masomo mwezi Januari. **Hakika Rais Samia anaandika historia nyingine kubwa nchini ya kuwezesha wanafunzi waliofaulu Mtihani wa darasa la 7 mwaka 2021 wote kuchaguliwa kuanza muhula wa masomo siku moja, January 2022**. Na hivyo kuzika rasmi utaratibu wa kuchagua wanafunzi wa kidato cha kwanza kwa awamu mbili. Hivyo kwa mwaka 2022 hakuna chaguo la pili la wanafunzi wa kidato cha kwanza.

Ndugu Wananchi, Natoa wito kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Viongozi na Watendaji wa Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa elimu kuhakikisha **kuwa wanafunzi wote waliochaguliwa wanaanza masomo yao mwezi Januari, 2022 bila vikwazo vya aina**

yoyote ili kutekeleza azma ya Serikali ya utoaji wa Elimumsingi Bila Malipo. Jambo hili litafanikiwa endapo kila mmoja kwa nafasi yake atawajibika katika kusimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa unaoendelea sasa hivi ili uweze kukamilika kwa wakati kama tulivyojipangia.

Hivyo, Ninawaagiza Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha ujenzi wa miundombinu yote kwa ajili ya kuwapokea wanafunzi wa Kidato cha kwanza mwaka 2022 **inakamilika kabla au ifikapo tarehe 15 Desemba 2021** kama nilivyoelekeza ili kuhakikisha wanafunzi wote wanaripoti shuleni kwa wakati ifikapo tarehe 15 Januari, 2022 kwa wanafunzi wa Bweni na tarehe 17 Januari, 2022 kwa wanafunzi wanaosoma shule za kutwa.

Vilevile, ninawahimiza, wazazi/walezi na jamii kushirikiana na uongozi wa Wilaya, Halmashauri na Shule, kuhakikisha kuwa wanafunzi wote waliochaguliwa wanaandikishwa, wanahudhuria na kubakia shuleni hadi watakapohitimu Elimu ya Sekondari.

Ndugu Wananchi, Orodha ya Wanafunzi wote waliochaguliwa pamoja na fomu za maelezo ya mahitaji ya kujiunga na Kidato cha Kwanza (*Joining Instructions)* kwa shule zote za Bweni za Kitaifa zinapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI

kupitia kiunganishi cha ***www.tamisemi.go.tz*** *na* Baraza la Mitihani ***www.necta.go.tz*****.**

Ndugu Wananchi, Pamoja na maelekezo haya, kwa mwanafunzi, mzazi/mlezi atakayekuwa na suala linalohitaji maelekezo au ufafanuzi zaidi aende katika Ofisi za Elimu za Mikoa na Halmashauri au apige

simu kwenye namba ya Kituo cha Huduma za Wateja, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa namba za simu **026 2160210** au **0735 160210**.

AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA

Ummy A. Mwalimu (Mb)
WAZIRI WA NCHI, OR - TAMISEMI

24 Novemba, 2021